Mtokambali.

waumini wa dini zote, hivyo hawapaswi



Naibu Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega (kushoto) akikabidhi vifaa vya kutakasa mikono kwa Mkuu wa Wilaya ya Longido, Franck Mwaisumbe, wilayani humo, mkoani Arusha jana, kwa ajili ya kuweka katika maeneo ya minada ya mifugo, ili kuwakinga wafanyabiashara dhidi ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

Scanned by CamScanner



**KUPIMA JOTO: MKUU wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa (kushoto), akipimwa joto na Ofisa Afya wa Kituo cha Magaoni, Farida Mohamed, kabla ya kuingia kwenye kikao cha Baraza la Madiwani ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga juzi.**

ARUSHA

# Serikali yasisitiza kutofunga minada

**Na JANETH MUSHI**

TANGA

# Watanzania watakiwa kutumia vizuri muda huu kuabudu

**Na AMINA OMARI**

Scanned by CamScanner

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Tobias Mwilapwa (katikati), akizungumza na wamiliki na wahudumu wa ... baada ya kupokea vifaa vya maji ya kunawia mikono, vilivyotolewa na chama cha ... Tanga, (Taremaj), kwa ajili ya kuviweka katika vituo vya mabasi jijini humo, jana. PICHA: DEGE MASOLI

# Serikali yatoa masharti minada ya mifugo

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

SERIKALI imeagiza viongozi walipo kwenye mikoa ya wafugaji nchini, kuhakikisha maeneo ya minada ya mifugo inaendelea bila kuwapo kwa mikusanyiko ya watu wengi.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ikiwa ni hatua ya kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa corona.

Ulega alitoa agizo hilo alipotembelea soko la kimataifa la mifugo, lililoko mpakani mwa Tanzania na Kenya wilayani Longido na eneo la minada wa mifugo lililoko eneo la Meserani wilayani Monduli.

Alisema ni lazima biashara na shughuli za kiuchumi ziendelee ili serikali ipate mapato huku familia zikipata mahitaji yao muhimu.

"Hatuwezi kufunga minada hii kwa sababu maisha ya Watanzania walio wengi inategemea kwa kufanya mambo ya kila siku, hivyo kuacha minada hii ni sawa na kutaka wafe kwa njaa. Sasa hili serikali tumelitafakari kwa kina na tumeona haifai kufunga minada hii," alisema.

Naibu Waziri alisisitiza kila mmoja kuhakikisha anachukua tahadhari anapokuwa eneo la minada ikiwa ni pamoja na kupunguza msongamano wa watu.

"Ninachosisitiza hapa kwenye minada hii wawepo tu wale wanaouza mifugo na wanaonunua, lakini mkishamaliza tu ondokeni mara moja minadani na sitaki muweke mikusanyiko na katika hili naomba mlizingatie," alisema.

Ulega alipongeza minada hiyo aliyotembelea kukuta wamechukua tahadhari kwa kuweka vitakasa mikono na maji tiririka pamoja na kuhakikisha kila anayeingia eneo hilo ananawa mikono yake.

Pia aliagiza kwa yeyote atakayekaidi kunawa kwa hiari achukuliwe hatua kali ili kunusuru afya yake na watu wanaomzunguka.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frank Mwaisumbe, alishukuru serikali kuruhusu wananchi wake kuendelea na minada ya mifugo, sababu ni sehemu ya maisha yao.

"Mwanzoni ugonjwa huu ulivyoingia tulisimamisha kidogo biashara hii na kuona taharuki kwa wafugaji wetu, lakini baadaye Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa aliwasiliana na viongozi wenzake wa nchi jirani ya Kenya na kuturuhusu kuendelea na minada yetu.

> NI LAZIMA BIASHARA NA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZIENDELEE ILI SERIKALI IPATE MAPATO HUKU FAMILIA ZIKIPATA MAHITAJI YAO MUHIMU.

Kwa kweli wanakuja Wakenya wengi katika soko letu la kimataifa la hapa mpakani Namanga kununua mifugo," alisema.

Kuhusu tahadhari, alisema wanachukua zote ili kuhakikisha kila anayeingia katika eneo hilo anakuwa salama dhidi ya ugonjwa huo.

Nao wafanyabiashara wa mifugo, Solomon Laizer na Lomnyaki Mollel, walishukuru kuruhusiwa kuuza mifugo yao na kuomba serikali kuweka vipima joto kwenye minada yao ili kila atakayeingia apimwe na atakayebainika kuwa na shida asiruhusiwe kuingia minadani.

# Abambwa akiuza mafuta kwenye chupa

uk 8

daa vituo
hifadhi
va corona

bao unapakana na
ya Congo (DRC) na
oka nchi za Burundi
vituo 13 kwa ajili ya
raia wa nchi za nje
hi hatua za kujikinga na
wa wa corona.
na na Mkuu wa
Homera, wakati wa
mati ya Afya ya Msingi,
ika kwenye ukumbi wa
a Mpanda.
huo umeweka mikakati
ujikinga, kujiadhari na
a ugonjwa wa virusi

kuwa ukipokea wageni
nda na Burundi, hivyo
a vituo 13, ambavyo
ageni wanaotoka nchi
a na ugonjwa huo.
iagiza kamati zote za
a, kuhakikisha kwenye
gia ndani ya mkoa huo,
e vizuizi hivyo viwepo
usalama.

anaofika
uu kwa
eza miradi
aendeleo
i wa
kikishe
chunguzi

a wa Katavi,
mera

wanaofika kwenye
... kutekeleza miradi

**Mikakati>>** Hoteli 12 zatengwa kwa watakaowekwa karantini

# *Mpina aitaka Takukuru kumulika upigaji bil.2. 6/- maabara ya uvuvi*

**NA MWANDISHI WETU**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ameitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kumulika upigaji wa sh. bilioni 2.6, katika ujenzi wa maabara ya kisasa ya uvuvi.

Kutokana na hilo, Waziri Mpina amesimamisha malipo yote kwa mkandarasi wa Kampuni ya Petra Construction Co. Limited, inayojenga maabara hiyo ya kisasa ya Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI), kituo cha Dar es Salaam, hadi uhakiki wa gharama halisi za mradi huo utakapokamilika.

Hatua hiyo imekuja baada ya waziri huyo kubaini uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma sh. bilioni 2.6

Waziri Mpina ameunda tume ya kiuchunguzi itakayofanya kazi kwa siku saba na kuwahusisha wataalamu kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kubaini ukweli wa gharama halisi za mradi huo.

Akizungumza baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI), Dar es Salaam, Waziri Mpina alisema amebaini mradi unaojengwa miundombinu yake ni midogo, ikilinganishwa na mkataba ulioridhiwa wa sh. bilioni 2.6.

Alisema taarifa ya uhakiki ya mradi huo, itawasilishwa wizarani ikiwa na mapendekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya wizi huo wa fedha za umma.

Waziri Mpina alisema thamani halisi ya mradi huo hailingani na fedha zilizotolewa na serikali huku akitolea mfano baadhi ya miradi ya ujenzi wa majengo mbalimbali, ikiwemo vituo vya afya na hospitali za wilaya zinazojengwa maeneo mbalimbali nchini.

Hata hivyo, wakati mjadala ukiendelea wa kuhoji matumizi ya fedha hizo kwenye mradi huo, mmoja wa wakandarasi wanaojenga majengo hayo, alimweleza Waziri Mpina kuwa, hadi mradi utakapokamilika, kutabaki 'chenji' sh. milioni 500, jambo lililotilia shaka na kuibua maswali mengi juu ya gharama halisi za mradi huo.

Kutokana na mkanganyiko huo wa maelezo ya mkandarasi na hali halisi iliyoonekana kwenye mradi huo, Waziri Mpina alilazimika kutangaza uamuzi huo wa kuundwa tume hiyo, ili ifanye tathmini ya gharama ya mradi iliyofanywa na mshauri mwelekezi wa mradi, namna zabuni ya kumpata mkandarasi ilivyotangazwa na namna mshauri mwelekezi alivyopatikana na hali ya ujenzi unavyoendelea kwa sasa ili kujua dosari ilisababishwa na nani.

Alisema baada ya kazi hiyo ya uhakiki kukamilika ndani ya siku saba, ukweli utajulikana na hatua zote zilizopitiwa katika mradi huo ili kubaini kama Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, ilikiukwa ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa wote watakaohusika na ubadhirifu huo wa fedha za umma.

"Sikubaliani na hizi gharama za mradi, majengo na miundombinu ni midogo, ikilinganishwa na mkataba wa bilioni 2.6, BOQ ulihakikiwa na wahandisi wa wizara, washauri waelekezi walijiridhisha kwamba iko sawa na ujenzi ukaenda hadi bilioni 2.6, mtu yeyote akija anakataa," alihoji Waziri Mpina

Aliagiza ujenzi wa mradi huo uendelee bila kusimama na ukamilike Aprili 20, mwaka huu, kama mkataba unavyoeleza na baada ya jengo jyzinduliwa, ikiwa ni sehemu ya kuleta mageuzi makubwa ya sekta ya uvuvi kupitia eneo hilo muhimu la utafiti.

"Nitaleta timu ya ukaguzi itakayofanya uhakiki wa thamani ya fedha katika ujenzi wa jengo hili, kuanzia kwenye kutangaza tenda yenyewe, thamani ya mradi, kumpata mkandarasi mwenyewe, mkadirio ya gharama zilizofanywa na wizara na baadae watafanya uhakiki wa kinachoendelea kujengwa hapa na kujua thamani halisi inayotakiwa na kwanini mradi huu upitishwe hadi kusainiwa," alisema Waziri Mpina.

Meneja wa Mradi wa Swiofish, Flora Luhanga, alisema mradi huo wa ujenzi wa Jengo la Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ulianza Juni 10, 2019, kwa gharama ya sh. bilioni 2, 609,491,754, unajengwa na mkandarasi, Kampuni ya Petra Construction Limited na kusimamiwa na kampuni ya YP Architect.

Luhanga alisema mradi huo unajumuisha pia ujenzi wa uzio, ofisi ya walinzi, kuchimba kisima cha maji, ujenzi wa tenki la maji ya mvua na kujenga mnara wa maji.

Mkandarasi wa mradi huo, Nicholaus Mlayi, alisema hadi sasa ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 70 na tayari ameshalipwa sh. milioni 963 na unatarajia kukamilika Aprili, mwaka huu.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Uvuvi, Magese Bulayi, alimhakikishia Waziri Mpina kuwa, maagizo yote aliyoyatoa atayasimamia kikamilifu, hasa katika kuangalia thamani ya fedha katika mradi huo na kwamba, hatua stahiki zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kuhusika katika mchakato huo.

**FEDHA ZA WAKULIMA**

Scanned by CamScanner

# Waziri Mpina asimamisha malipo ya mkandarasi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina amesimamisha malipo yote kwa Mkandarasi wa Kampuni ya Petra Construction Co. Limited inayojenga maabara ya kisasa ya Taasisi ya Uvuvi Tanzania (TAFIRI) kituo cha Dar es Salaam hadi uhakiki wa gharama halisi za mradi huo utakapokamilika.

Hatua hiyo imekuja baada ya kubaini kuwepo matumizi mabaya ya fedha za umma kiasi cha sh. bilioni 2.6.

Akizungumza mara baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) jijini Dar es Salaam juzi, Waziri Mpina alisema amebaini mradi unaojengwa miundombinu yake ni midogo ikilinganishwa na mkataba uliondhiwa wa sh. bilioni 2.6.

Aliagiza taarifa ya uhakiki ya mradi huo iwasilishwe wizarani ikiwa na mapendekezo ya hatua za kuchukua dhidi ya wizi huo wa fedha za umma.

Waziri Mpina ameunda tume ya uchunguzi itakayofanya kazi kwa siku saba na kuwahusisha wataalamu kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kubaini ukweli wa gharama halisi za mradi huo.

Waziri Mpina alisema thamani halisi ya mradi huo hailingani na fedha zilizotolewa na Serikali huku akitolea mfano baadhi ya miradi ya ujenzi wa majengo mbalimbali ikiwemo vituo vya afya na hospitali za wilaya zinazojengwa maeneo mbalimbali nchini.

Hata hivyo wakati wa mjadala ukiendelea wa kuhoji matumizi ya fedha hizo kwenye mradi huo, mmoja wa wakandarasi wanaojenga majengo hayo alimweleza Waziri Mpina kuwa hadi mradi utakapomika kutabaki 'chenji' kiasi cha sh. milioni 500 jambo lililoleta mashaka na kuibua maswali mengi juu ya gharama halisi za mradi huo.

Kufuatia mkanganyiko huo wa maelezo ya mkandarasi na hali halisi iliyoonekana kwenye mradi huo ndipo Waziri Mpina akalazimika kutangaza uamuzi huo wa kuundwa tume hiyo ili iweze kufanya tathmini ya gharama ya mradi iliyofanywa na Mshauri mwelezi wa mradi, namna zabuni ya kumpata mkandarasi ilivyotangazwa na namna mshauri mwelekezi alivyopatikana na hali ya ujenzi unavyoendelea kwa sasa ili kujua dosari ilisababishwa na nani.

Hivyo Waziri Mpina alibainisha kuwa baada ya kazi hiyo ya uhakiki kukamilika ndani ya siku saba ukweli utajulikana na hatua zote zilizopitiwa katika mradi huo ili kubaini kama Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004 ilikiukwa ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa wote watakaohusika na ubadhirifu huo wa fedha za umma.

"Sikubaliani na hizi gharama za mradi majengo na miundombinu ni midogo ikilinganishwa na mkataba wa bilioni 2.6, BOQ ilihakikiwa na wahandisi wa wizara, washauri waelekezi walijirdhisha kwamba iko sawa na ujenzi ukaenda hadi bilioni 2.6 mtu yeyote akija anakataa," alihoji Waziri Mpina

Hivyo Waziri Mpina ameagiza ujenzi wa mradi huo uendelee bila kusimama na ukamilike ifikapo Aprili 20 mwaka huu kama mkataba unavyoeleeza na baada ya jengo litazinduliwa ikiwa ni sehemu ya kuleta mageuzi makubwa ya sekta ya uvuvi kupitia eneo hilo muhimu la utafiti.

"Nitaleta timu ya ukaguzi itakayofanya uhakiki wa thamani ya fedha katika ujenzi wa jengo hili, kuanzia kwenye kutangaza tenda yenyewe, thamani ya mradi, kumpata mkandarasi mwenyewe, cost estimates zilizofanywa na wizara na baadae watafanya uhakiki wa kinachoendelea kujengwa hapa na kujua thamani halisi inayotakiwa na kwanini mradi huu upitishwe hadi kusainiwa," alihoji Waziri Mpina.

Meneja wa Mradi wa Swiofish, Flora Luhanga alisema mradi huo wa ujenzi wa Jengo la Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi ulianza Juni 10, 2019 kwa gharama ya shilingi bilioni 2, 609,491,754 unajengwa na Mkandarasi Kampuni ya Petra Construction Limited na kusimamiwa na Kampuni ya YP Architect.

Luhanga alisema mradi huo unajumuisha pia ujenzi wa uzio, ofisi ya walinzi, kuchimba kisima cha maji, ujenzi wa tenki la maji ya mvua na kujenga mnara wa maji.

Mkandarasi wa Mradi huo, Nicholaus Mlayi alisema hadi sasa ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 70 na tayari ameshalipwa shilingi milioni 963 na unatarajia kukamilika mwezi Aprili.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Uvuvi, Magese Bulayi alimhakikishia Waziri Mpina kuwa maagizo yote aliyoyatoa atayasimamia kikamilifu hasa katika kuangalia thamani ya fedha 'value for money' katika mradi huo na kwamba hatua stahiki zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kuhusika katika mchakato huo.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina (katikati) akipata maelezo ya namna ya shughuli ya ujenzi wa mradi wa jengo la Maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Kituo cha Dar es Salaam kutoka kwa Mkandarasi wa Kampuni ya Petra Construction Limited, Nicholaus Mlayi alipotembelea mradi huo Kunduchi, Dar es Salaam.** (Na Mpigapicha Wetu)

## Taasisi zaombwa kuchangia vifaa kusaidia vita dhidi Corona

**Na Mwandishi Wetu, Arusha**

TAASISI na makampuni binafsi zimeaombwa kuchangia vifaa mbalimbali kwa ajili ya kusaidia kupambana na ugonjwa wa Corona, ambao umeleta mtikisiko wa kiuchumi

Wataalam na makada wa afya zaidi ya 525, wamepewa mafunzo elekezi juu ya kukabiliana na ugonjwa huo wa Corona.

Rai hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Arusha, Hargeney Chitukuro wakati akifungua kikao kazi cha wataalamu wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii katika kutekeleza mkakati wa kuelemisha jamii kuhusu ugonjwa wa Corona kilichofanyika mkoani hapa.

Chitukuro alisema endapo taasisi na makampuni binafsi yakijitokeza kuchangia vifaa kwa ajili ya kupambana na ugonjwa huo, kutasaidia kuwapa ahueni wagonjwa watakaobainika kuwa na ugonjwa huo na kuwekwa karantini.

Alisema Hospitali ya Mount Meru,

Scanned by CamScanner

MAJIRA UK 8

## upimaji

vyo, ameishauri
ya wilaya ya Musoma
wataalamu wake kwa
iko ili kupatiwa mkopo
naotokewa na wizara
shughuli za umilikishaji
alisema katika kipindi
ayo wizara inatarajia
ii saba kwa ajili ya
almashauri.
de wake Mkuu wa
usoma Dkt Vincent
aliipongeza wizara
nba na Maendeleo
a uamuzi wake wa
za mikoa na kueleza
huo utaleta nafuu
hi wa mara katika
a za ardjhi ambapo
imu kusagiri hadi
a huduma hiyo.



## i imani

maalumu vya
kabla ya kuingia
kwenye taasisiza

nde wake Mkuu
nga Thobias
giza maafisa
mo kuhakikisha
eneo yote ya
wahakikisha
eo la kunawia
kabla ya kupata

taarifa ni wapi
ekeleza jambo
e taasisi zote
tolea huduma
nocheo kikubwa
kupambana na
ona," alisema.

# Wavuvi wachukua tahadhari ugonjwa wa Corona

**Na Judith Ferdinand, Mwanza**

WAVUVI wa Mwalo wa Butuja uliopo Wilayani Ilemela Mkoani Mwanza wamechukua tahadhari ya kujikinga na homa kali ya mapafu inayosababishwa na kirusi aina ya Corona (COVID-19) kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya kuweka vifaa vya kunawia mikono, maji tiririka na sabauni katika mwalo huo.

Akizungumza na gazeti la Majira jana lilipotembelea mwalo huo ili kuona hatua zilizochukuliwa za kujikinga na ugonjwa huo Katibu wa Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi ndani ya mita 60 kutoka mwambao wa ziwa,Emmanuel Nyagwesi, alisema katika kujikinga na Corona yeye kama kiongozi amechukua tahadhari kwa kuweka maji na sabubi eneo la kuingilia Mwaloni hapo ili kwa wavuvi na watu wanaofanya shughuli na wanaoenda kununua samaki hapo kabla ya kuingia wananawe mikono.

Nyagwesi, alisema mbali na kuweka vifaa vya kunawia mikono pia wamewaambia watu kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima angalau wakae watu wa tatu kwani Serikali imeagiza watu wasisongamane na wao wametii masharti.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa wa Mtaa wa Butuja Kichonge Mwita, alisema wanahimiza watu kufuata maagizo na maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya namna ya kujikinga na ugonjwa huo huku wakiendelea kuelimisha watu.

"Tumechukua tahadhari, tumeweka maji kwenye kona za kuingilia maeneo haya ili basi watu wanaokuja kutembelea na kupata huduma katika eneo hili kutoka sehemu mbalimbali pamoja na wavuvi waweze kunawa kwanza mikono kabla ya kuingia ndani ya mwalo, tunaendelea kuwaambia kuwa mikusanyiko haitakiwi pia hata mikutano ya hadhara na mambo mengine yote yenye mikusanyiko tumesitisha," alisema Mwita.

Pia Mwita, aliomba Serikali kuendelea kuelimisha watu kwani ugonjwa huu ni mbaya sana,na wao viongozi wa Serikali za mitaa wameshapokea maelekezo kutoka kwa viongozi wa juu na tuombe Mungu anaweza kusaidia jambo hili likaisha.

Naye mmoja wa watu wanaofanya shughuli katika mwalo huo Cyprian Chacha, alisema wamejipanga vizuri katika kujikinga na Corona kwa kuweka maji na sabuni pamoja na kamba ambayo inatumika kumzuia mtu kuingia mwaloni hapo bila kunawa mikono.

Scanned by CamScanner

iko

kusanyika katika
mbo ambalo ni
na hatua hiyo,
atua za kuzifun-
a ziada zilizoku-
cho pamoja na
ezo mbalimbali
utekelezaji wa

ri ndiyo maana
ngozi wenzangu
kuu wa wilaya
u ya tahadhari
na na ninashuk-
neonyesha utii,"

ilo litakuwa en-
anchi wa shehia
jumuika katika
kwa sasa ili ku-
ya maradhi ya
uchukua tahad-



i mjini Zanzi-
i vya corona,

ni

ria na kufanya
ikiwamo rasmi
nchini.
kufahamu wa-
aeneo yao na
afya zao kabla
i.
doria katika
a pwani wote
sio rasmi, lak-
hi kinyume na

methibitishwa
ea Mombasa
mjini na Tun-
hofia ugonjwa

# Uvuvi haramu wapungua hifadhi ya bahari

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

IDARA ya Maendeleo ya Uvuvi ya Serikali ya Zanzibar imesema uvuvi haramu kwa kutumia mabomu umepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia doria zinazofanywa mara kwa mara katika maeneo ya ukanda wa hifadhi ya bahari ya Zanzibar.

Mkuu wa doria wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Haji Shomari, alisema hayo wakati wa kufanya doria katika ghuba ya hifadhi ya Minai inayounganisha eneo la Mkoa wa Kaskazini hadi Kusini Unguja.

Alisema uvuvi haramu wa kutumia mabomu kwa kiasi kikubwa ulikuwa ukifanywa kwa kuwashirikisha wavuvi kutoka nje ya visiwa vya Zanzibar.

Shomari alisema uvuvi huo ulikuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa matumbawe ambayo baadhi yake yamekufa kwa kushambuliwa na mabomu.

Vile vile, alisema katika kipindi cha miaka miwili 2018-2019 wamefanikiwa kufanya doria 1,532 ambazo hakuna wavuvi waliokamatwa wanaotumia mabomu.

"Tumefanya doria katika maeneo ya hifadhi ya ukanda wa bahari ya Zanzibar kwa muda mrefu sasa na tumebaini kwamba uvuvi wa kutumia mabomu umetoweka...tunashukuru kwa sababu athari zake ni kubwa sana," alisema.

Alitaja aina nyingine za uvuvi haramu ambao umepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia kuimarishwa kwa doria ni wa kutumia nyavu za kukokota pamoja na bunduki.

Alisema uvuvi huo umepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ushirikiano wa kamati za uvuvi za shehia mbalimbali za Unguja na Pemba.

"Tunazipongeza kwa kiasi kikubwa kamati za uvuvi za shehia za hifadhi kwa kazi kubwa ya kupambana na uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi kwa lengo la kupata kipato kikubwa," alisema.

**"Tumefanya doria katika maeneo ya hifadhi ya ukanda wa bahari ya Zanzibar kwa muda mrefu sasa na tumebaini kwamba uvuvi wa kutumia mabomu umetoweka...tunashukuru kwa sababu athari zake ni kubwa sana," alisema.**

# Kliniki 10 za mifugo sasa kujengwa kwenye h/shauri

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIKA mwaka wa fedha wa 2020/21, serikali imejipanga kujenga kliniki za mifugo 10 kwenye halmashauri mbalimbali nchini ikiwamo Singida Vijijini.

Hayo yalibainishwa jana bungeni katika majibu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi katika swali la Mbunge wa Singida Kaskazini(CCM), Justine Monko.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali wa kuongeza wataalamu ama vitendea kazi kama njia mbadala ya kuwasaidia wataalamu wachache waliopo kutoa huduma bora kwa wafugaji.

"Ni lini serikali itajenga maabara za mifugo katika maeneo ya wafugaji ili wananchi waache kutibu mifugo kwa kubahatisha?" Alihoji.

Monko alisema mifugo ya wafugaji wakubwa nchini imekosa ubora wa mazao yake kutokana na maradhi yanayochangiwa na kukosekana kwa wataalamu waliobobea katika fani na kukosa maabara za mifugo.

"Je, ni lini serikali itajenga maabara za mifugo katika maeneo ya wafugaji?" Alihoji Monko.

Kwa muhibu wa majibu yaliyotolewa na Wizara ya Mifugo, serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa maabara za mifugo kwenye kila mkoa.

"Mpaka sasa kuna maabara za mifugo za serikali 11 kwenye kila kanda," ilisema.

Aidha, wizara imeshavielekeza vituo binafsi 1,709 vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vilivyopo kwenye halmashauri zote 185 kuhakikisha vinakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kutoa huduma ya uchunguzi wa awali wa magonjwa ya mifugo.

Pia inafanya juhudi za kuongeza idadi ya maofisa ugani wa mifugo kwa kuiwezesha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) kuongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada katika fani za uzalishaji, afya ya mifugo, nyanda za malisho na maabara.

Wizara hiyo ilibainisha kuwa wanafunzi hao wameongezeka kutoka wanafunzi 2,536 mwaka 2018/2019 hadi mwanafunzi 3,634 mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la wanafunzi 1,098.

Scanned by CamScanner

ya watu.
Mwito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazee Zanzibar (Juwaza),

kuchukua tahadhari ya kujikinga ili wasivipate.
"Mzee mwenye umri wa miaka 70 kinga zake za


wenyeumri
alisema.
Awali, Ka
wa Juwaza, S
aliwapongez

HABARI LEO UK 19

# * Uvuvi wa kutumia mabomu wapungua

IDARA ya Maendeleo ya Uvuvi ya Serikali ya Zanzibar imesema, uvuvi haramu wa kutumia mabomu umepungua kwa kiasi kikubwa, kutokana na doria zinazofanywa mara kwa mara katika maeneo ya Ukanda wa Hifadhi ya Bahari ya Zanzibar.

Mkuu wa doria wa idara hiyo, Haji Shomari, alisema hayo wakati alipofanya doria katika ghuba ya hifadhi ya Minai inayojumuisha eneo la mkoa wa Kaskazini hadi Kusini Unguja.



Alisema uvuvi wa haramu wa kutumia mabomu kwa kiasi kikubwa ulikuwa ukifanywa na wavuvi kutoka nje ya visiwa vya Zanzibar.

Shomari alisema uvuvi huo ulikuwa chanzo kikubwa cha uharibifu wa matumbawe ambayo baadhi yake yamekufa kwa kushambuliwa na mabomu.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili 2018-2019, wamefanikiwa kufanya doria 1,532, ambazo hakuna wavuvi waliokamatwa wanaotumia mabomu.

"Tumefanya doria katika maeneo ya hifadhi ya Ukanda wa Bahari ya Zanzibar kwa muda mrefu sasa na tumebaini kwamba uvuvi wa kutumia mabomu umetoweka, tunashukuru kwa sababu athari zake ni kubwa sana," alisema.

Aidha, alitaja aina nyingine za uvuvi haramu ambao umepungua kwa kiasi kikubwa kufuatia kuimarishwa kwa doria ni wa kutumia nyavu za kukokota pamoja na bunduki.

Alisema uvuvi haramu kwa ujumla umepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na ushirikiano mkubwa wa kamati za uvuvi za shehia mbalimbali zilizopo Unguja na Pemba.

"Tunazipongeza kwa kiasi kikubwa kamati za uvuvi za shehia za hifadhi kwa kazi kubwa ya kupambana na uvuvi haramu unaofanywa na wavuvi kwa lengo la kupata kipato kikubwa," alisema.

Pia aliipongeza serikali ya Zanzibar kwa kununua boti tatu za kisasa kwa ajili ya kufanyia doria maeneo ya ukanda wa hifadhi ya bahari ya Unguja na Pemba.

Mkuu wa mradi wa usimamizi wa uvuvi wa Kanda ya Kusini na Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOfish) kwa upande wa Zanzibar, Hashim Moumin, alisema lengo la mradi huo ni kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia masuala ya uvuvi ili kuimarisha uvuvi endelevu.

Alisema uvuvi endelevu utafanikiwa kama jamii ya wavuvi itaendesha shughuli zao kwa kuzingatia na kuweka kipaumbele cha uvuvi wenye tija unaozingatia mazingira.

"Ndiyo maana katika mradi wa SWIOfish suala la doria katika maeneo ya hifadhi limepewa kipaumbele kuona kwamba uvuvi haramu unadhibitiwa na kuyafanya matumbawe kuwa salama zaidi,"

# * Ma kuc

WA m Pe na kamati z usalama za wametakiw uingiaji wa la kutoka nj hicho, ikiwa ya kudhibit zi mapya ya corona.

Waziri wa Rashid, alito jana akiwa k mikoa miwil hicho na kut za Tundauw ambazo hup kutumiwa n



Waziri wa N la Makundu Muyuni Mko kuhusu kujik




# Maabara za mifugo kujengwa kila mkoa

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina amesema serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa maabara za mifugo kwenye kila mkoa.

Pia amesema udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na shaahada katika fani mbalimbali za afya ya mifugo imeongezeka kwa asilimia 43.3.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina wakati wa kujibu swali la msingi la Mbunge wa Singida Kaskazini, Justine Monko (CCM) aliyetaka kujua mpango wa Serikali katika kuongeza wataalam ama vitendea kazi kama njia mbadala ya kuwasaidia wataalamu wachache waliopo kutoa huduma bora kwa wafugaji.

Pia alitaka kujua ni lini Serikali itajenga maabara za mifugo katika maeneo ya wafugaji ili wananchi waache kutibu mifugo yao kwa kubahatisha.

Akijibu swali hilo, Mpina alisema Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa maabara za mifugo kwenye kila mkoa.

Alisema mpaka sasa kuna maabara za mifugo za Serikali kumi na moja kwenye kila Kanda.

"Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara inategemea kujenga Kliniki za mifugo zenye maabara katika halmashauri mbili za Chato na Meatu.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imepanga kujenga Kliniki zingine 10 kwenye Halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Sindiga Vijijini.

Mpina alisema Wizara pia imeshavielekeza vituo binafsi 1,709 vya kutolea huduma ya afya ya mifugo vilivyopo kwenye Halmashauri zote 185 kuhakikisha vinakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kutoa huduma ya uchunguzi wa awali wa magonjwa ya mifugo.

Aidha, Mpina alisema katika kuhakikisha kunakuwa na ongezeko la maafisa ugani wa mifugo, Serikali imejikita kuongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya astashahada na stashahada wa fani mbalimbali afya ya mifugo kwa asilimia 43.3.

# Ma ku

WA S A amelithibit Serikali kw na mahaka lea kuonge hakimu ka kupunguz mashauri r

Balozi M hayo akijibu mbunge wa mani Ally Y

Katika sv Dk Yussuf a mahakama tibu wa kua mashauri ar



Wabunge kwa vikao

# Dk Mpango: W

...kishwa kortini jana.

...Hospitali ya Mkoa wa Mara, Kazoba Wilson (kushoto) mjini Musoma jana. Kulia kwake ni Mkuu wa ...Mabula akipata maelezo kutoka kwa Mhandisi wa Wilaya ya Musoma, Dk Vincent Anney. (Na Mpigapicha Wetu).

# Ulega aagiza minada ya mifugo isifungwe


**Na Veronica Mheta, Longido**

NAIBU Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega ameagiza viongozi waliopo kwenye mikoa ya wafugaji nchini, kuhakikisha katika maeneo ya minada ya mifugo inaendelea bila kuwepo mikusanyiko ya watu wengi, pamoja na kuchukua tahadhari ya virusi vya corona.

Ulega alitoa agizo hilo jana alipotembelea soko la kimataifa la mifugo lililopo mpakani mwa Tanzania na Kenya wilayani Longido na eneo la mnada wa mifugo Meserani wilayani Monduli.

Alisema ni lazima biashara na shughuli za kiuchumi ziendelee ili serikali ipate mapato, huku familia zikipata mahitaji yao muhimu.

"Hatuwezi kufunga



minada hii sababu maisha ya Watanzania wengi ni kutafuta mlo wa kila siku, hivyo kuzuia minada hii ni sawa na kutaka wafe kwa njaa. Serikali tumelitafakari kwa kina na tumeona haifai kufunga minada hii," alisema.

Alisema kikubwa ni kila mmoja kuchukua tahadhari awapo eneo la mnada na kupunguza msongamano wa watu ili wasiambukizane.

"Hapa kwenye minada wawepo wale wanaouza mifugo na wanaonunua, lakini mkishauziana tu ondokeni mara moja mnadani na sitaki muweke mikusanyiko. Naomba hili mlizingatie," alisema.

Ulega aliagiza pia kwa yeyote atakayekaidi kunawa kwa hiari achukuliwe hatua kali ili kunusuru afya yake na watu wanaomzunguka.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frenk Mwaisumbe alishukuru serikali kuruhusu wananchi kuendelea na minada ya mifugo.

"Awali ugonjwa huu ulivyoingia tulizuia kidogo biashara hii na kuzua taharuki kwa wafugaji lakini baadaye Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliwasiliana na viongozi wa Kenya na kuruhusu kuendelea na minada yetu na kweli wanakuja Wakenya wengi katika soko letu la kimataifa la mpakani Namanga kununua mifugo," alisema.

Kuhusu tahadhari alisema wanachukua zote, ili kuhakikisha kila anayeingia anakuwa salama.

Scanned by CamScanner